



Mwongozo wa Duka Langu

Jifunze kutumia mfumo hatua kwa hatua: kuuza, kusimamia stock, kuandika matumizi, na kuelewa faida na hasara ya biashara yako.

1 Kuanza

Hatua tatu tu kabla ya kuuza bidhaa ya kwanza.

1 Ingia kwenye mfumo

Tumia barua pepe (au namba) na nywila ulizopewa. Ukitaka mfanyakazi aingie, mwongeze kama mtumiaji kulingana na kifurushi chako.

2 Weka bidhaa zako

Kwa kila bidhaa weka jina, bei ya kununulia, bei ya kuuzia na idadi uliyonayo. Unaweza kupakia orodha nyingi kwa CSV, na kutumia barcode au QR.

3 Anza kuuza

Fungua POS, chagua bidhaa, pokea malipo. Mfumo unapunguza stock na kuhesabu faida wenyewe.



Bei ya kununulia ni muhimu. Ndiyo inayowezesha mfumo kujua faida halisi ya kila mauzo. Ukiiacha tupu au ukaiandika vibaya, faida itaonekana kubwa au ndogo kuliko ukweli.

2 Kuuza (POS)

Chagua bidhaa, kipokee malipo, na umemaliza. Kila kitu kingine kinatokea chenyewe.



Njia za malipo

Taslimu

Pesa mkononi. Inaingia moja kwa moja kwenye hesabu ya pesa.

M-Pesa / simu

Weka njia ya malipo uliyopokea ili ripoti ya pesa ibaki sahihi.

Mkopo (deni)

Mteja anachukua sasa, analipa baadaye. Mauzo yanaandikwa, na deni linafuatiliwa kwenye ukurasa wa madeni.

Mengine unayoweza kufanya

- **Punguzo:** mfumo unahesabu faida baada ya punguzo, kwa hiyo faida inayoonekana ni ya kweli.
- **Marejesho:** mteja akirudisha bidhaa, rekodi marejesho ili stock na pesa zirekebishwe.
- **Bili / tabs:** shika bili ya mteja ukihudumia mwingine, kisha urudi kuimaliza.
- **Offline:** mauzo ya kawaida yanaendelea hata mtandao ukikatika.

3 Stock na Write-off

Stock inapungua pale unapouza. Wakati mwingine bidhaa inatoka bila kuuzwa. Hapo ndipo unapotumia **Write-off**.

Write-off ni nini?

Ni kuondoa bidhaa kwenye stock **bila kuiuza**: imeharibika, imepotea, imeisha muda, au umeitumia mwenyewe ofisini. Kwenye ukurasa wa Stock, bonyeza **Toa Stock** na

uchague sababu.

SABABU	MFANO
Matumizi ya Ofisi	Ream ya karatasi uliyotumia ofisini
Iliharibiwa	Bidhaa iliyovunjika au kulowa maji
Upotevu	Bidhaa haionekani wakati wa kuhesabu stock
Nyingine	Sababu isiyoingia hapo juu (andika maelezo)

Write-off inabadilisha nini?

 Stock inapungua	 Matumizi yanaongezeka kwa bei ya kununulia
 Faida inapungua	 Pesa taslimu haiguswi



Mfano: kalamu 3 zilizoununuliwa kwa TZS 1,000 kila moja, ukizitoa kama "Matumizi ya Ofisi", zinaandikwa kama matumizi ya **TZS 3,000**. Faida ya mwezi inapungua kwa kiasi hicho. Pesa kwenye droo haibadiliki, kwa sababu pesa ilitoka ulipozinunua.



Ukikosea write-off, unaweza kuihariri au kuifuta kwenye historia ya stock. Ukiifuta, stock inarudishwa.

Bidhaa zinazoisha muda

Kwa bidhaa zenye tarehe ya mwisho (dawa, vyakula), mfumo unakuonyesha zinazokaribia kuisha. Ikishaisha, tumia write-off ya expiry ili stock na faida zionyeshe ukweli.

4 Matumizi (gharama)

Kila shilingi inayotoka kwa ajili ya biashara iandikwe, na **aina** ichaguliwe. Hapo ndipo ripoti inaweza kukuonyesha pesa zinaenda wapi.



Aina ni ya lazima. Ukiongeza gharama mpya, mfumo unakulazimisha kuchagua aina. Inakusaidia kuepuka gharama zisizoeleweka kwenye ripoti.

AINA	UNAITUMIA LINI
Kodi	Kodi ya chumba au duka
Umeme & Maji	LUKU, bili ya maji
Mishahara	Malipo ya wafanyakazi
Usafiri	Nauli, usafirishaji wa mzigo
Internet, Bando & Simu	Bando, vocha, internet ya ofisi
Chakula & Vinywaji	Chakula na vinywaji vya ofisi au duka
Usafi & Ulinzi	Usafi wa duka, mlinzi
TRA, Leseni & Ada za Serikali	Kodi ya TRA, leseni, ada za halmashauri
Ada za Benki & Mitandao ya Simu	Makato ya benki na ya M-Pesa, Tigo Pesa na mengine
Vifaa vya Ofisi	Karatasi, kalamu, vifaa vidogo vya matumizi
Vifaa vya Kudumu	Kompyuta, printa, samani
Matengenezo	Kutengeneza vifaa au duka
Matangazo	Matangazo, mabango, vipeperushi
Stock Iliyotumika au Kupotea (Write-off)	Inaingia yenyewe unapofanya write-off. Usiandike mwenyewe.
Nyingine	Chochote kisichoingia kwingine. Itumie kwa nadra.



Usichanganye matumizi na pesa binafsi. Pesa unazochukua kwa matumizi ya nyumbani si gharama ya biashara. Ni "pesa za mmiliki" (drawings), na zinapunguza mtaji, si faida.

5

Faida si pesa taslimu

Swali linaloulizwa mara nyingi: *"Faida ni kubwa, lakini pesa niliyonayo ni ndogo. Imenda wapi?"*

Faida ni hesabu ya kitabuni: mauzo ukitoa gharama ya bidhaa na matumizi. Si pesa iliyokaa mkononi. Baada ya kupatikana, faida inaweza kuwa:

Faida ya TZS 100 (mfano)



Pesa taslimu / M-Pesa
iko mkononi au benki

Stock mpya
umenunua bidhaa za kuuza

Madeni ya wateja
umeuza, hawajalipa bado

Pesa za mmiliki
ulizochukua au vifaa vya kudumu

Mgawanyo ni wa mfano tu. Biashara yako itakuwa na asilimia zake.

Mlinganyo wa mtaji

$$\begin{array}{|c|c|c|c|c|c|c|} \hline \text{Mtaji wa} & & & & & & \\ \text{kuanzia} & + & \text{Faida} & + & \text{Mtaji} & - & \text{Pesa} \\ \text{ulipoanza} & & \text{tangu} & & \text{uliyoongeza} & & \text{ulizochukua} \\ & & \text{mwanzo} & & \text{baadaye} & & \text{(drawings)} \\ \hline \end{array} =$$

Mtaji wa sasa
kwenye Balance Sheet



Mtaji wa sasa ukiwa chini ya "mtaji wa kuanzia + faida", tofauti hiyo inaelezwa na **pesa ulizochukua**, mabadiliko mengine yaliyoandikwa, au gharama ambazo hazikuingizwa. Stock na madeni ya wateja hazipunguzi mtaji. Zinabadilisha tu *umbo* la mali, kutoka pesa kuwa bidhaa au deni.

Mahali pa kuangalia kila kimoja: **Balance Sheet** (mali, madeni, mtaji), **Akaunti za Pesa** (pesa halisi kwa kila njia), na ukurasa wa **madeni**.

6 Ripoti


Ripoti zinakuambia biashara inaendeleaje bila kuhesabu kwa mkono.

Faida na Hasara (P&L)

- **Mauzo:** jumla ya mauzo ya kipindi, baada ya punguzo.
- **Gharama ya bidhaa:** bei ya kununulia ya bidhaa ulizouza.
- **Faida ghafi:** mauzo ukitoa gharama ya bidhaa.
- **Matumizi:** kodi, umeme, mishahara na mengine uliyoandika.
- **Faida halisi:** faida ghafi ukitoa matumizi. Hii ndiyo faida yako ya kweli.

Safari ya Biashara Biashara na Premier

Inaonyesha faida au hasara **tangu siku ya kwanza**, mwezi kwa mwezi. Unaona mwezi ulioanza kupata faida, miezi yenye hasara, na kama biashara inakua.



- **Nguzo** ni faida ya kila mwezi: kijani ni faida, nyekundu ni hasara.
- **Mstari** ni jumla tangu mwanzo. Ukiwa juu ya sifuri, biashara iko kwenye faida kwa jumla.
- **Vitufe** vya "Miezi 12 ya mwisho", kila mwaka na "Yote" vinakuruhusu kuangalia kipindi unachotaka. Hukumu ya juu ("Tangu mwezi X una faida ya...") inabaki ya tangu mwanzo daima.



Mwezi wa sasa bado haujaisha, kwa hiyo unaweza kuonekana na hasara kwa muda. Hiyo ni kawaida. Subiri uishe ndipo uuhukumu.

Balance Sheet na Akaunti za Pesa

Balance Sheet inaonyesha unachomiliki (pesa, stock, madeni ya wateja), unachodaiwa, na mtaji. **Akaunti za Pesa** inaonyesha pesa halisi kwa kila njia (taslimu, M-Pesa, benki).

7 Madeni

Fuatilia nani anakudai, na wewe unamdai nani.



Madeni ya wateja

Mauzo ya mkopo yanaandikwa kwa jina la mteja. Mteja akilipa, rekodi malipo, na deni linapungua.



Madeni ya wasambazaji

Ukinunua mzigo kwa mkopo kupitia Purchase Order, deni linaandikwa na unaweza kulipa kwa awamu.

[Biashara na Premier](#)



Mauzo ya mkopo yanaongeza **mauzo** lakini si **pesa** hadi mteja alipe. Ndiyo sababu faida inaweza kuwa kubwa wakati pesa mkononi ni ndogo.

8 Maswali yanayoulizwa mara nyingi

Bonyeza swali kuona jibu.

Faida inaonyesha mamilioni, lakini pesa niliyanayo ni ndogo. Kwa nini?

Faida si pesa taslimu. Pesa inaweza kuwa imegeuka stock mpya, madeni ya wateja, vifaa vya kudumu, au umeichukua kama pesa za mmiliki. Angalia sehemu ya Faida si pesa taslimu na Balance Sheet.

Write-off inapunguza pesa yangu ya taslimu?

Hapana. Inapunguza stock na faida, lakini haiguswi pesa taslimu, kwa sababu pesa ilitoka ulipoinunua bidhaa.

Kwa nini mfumo unanilazimisha kuchagua aina ya matumizi?

Ili ripoti ikuonyeshe gharama zinaenda wapi (kodi, umeme, mishahara...). Matumizi bila aina hayasaidii kufanya maamuzi.

Mwezi huu unaonyesha hasara, je biashara inaanguka?

Si lazima. Mwezi unaoendelea haujaisha, na baadhi ya gharama (kodi, mishahara) huingia mapema. Angalia Safari ya Biashara kuona mwenendo wa miezi mingi, na kama jumla tangu mwanzo bado iko juu ya sifuri.

Nimekosea kuandika matumizi, nifanye nini?

Fungua ukurasa wa Matumizi, hariri gharama hiyo (tarehe, aina au kiasi) au ifute. Mfanyakazi wa kawaida (cashier) anaweza kufuta ndani ya dakika 20 tu baada ya kuiingiza.

Nitapata wapi msaada zaidi?

Tuma ujumbe kwa timu ya msaada kupitia kitufe cha WhatsApp chini ya ukurasa huu.